# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# OFISI YA RAIS – TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

**Namba za simu** **Shule ya Sekondari Julius Kambarage Nyerere,**
Mkuu wa Shule **0769209747** S.L.P 435,
Makamu Mkuu wa Shule **0765516413** TARIME.
Mtaaluma **0784436058/0759412429** **30/03/2022**

Mzazi/Mlezi wa ……………………………………………………………
S.L.P …………………
……………………………….

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI JULIUS KAMBARAGE NYERERE HALMASHAURI YA WILAYA TARIME MKOA WA MARA MWAKA 2022**

1. Nafurahi kukuarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika shule hii mwaka 2022 tahasusi ya …………. Shule ya sekondari **Julius Kambarage Nyerere** ipo umbali wa Kilometa 22 kutoka Tarime mjini barabara kuu iendayo Nyamwaga. Shule hii ni Bweni kwa Wasichana kidato cha Tano na Sita, na kutwa kwa kidato cha kwanza hadi cha nne. Ukitokea Mwanza unashuka Tarime mjini, ukifika Tarime mjini (stand kuu) kuna magari yaendayoNyamwaga/Nyamongo/Itiryo (nauli tsh 5000). Kwa wale wa kanda ya kaskazini (Arusha na Moshi), wakipitia njia ya mbugani Serengeti, kuna mabasi yanayofika Tarime kupitia Nyamongo.Ukipitia njia hii, shukia **Nyamwaga ,Unaweza kumuomba dereva wa gari akushushe kwenye kibao cha shule**.
2. Muhula wa masomo unaanza tarehe **--------------------** Hivyo unapaswa kuripoti shuleni kuanziatarehe **---------------------------------**

   **TANBIHI:** Mwanafunzi hatapokelewa endapo atachelewa zaidi ya wiki mbili tangu tarehe ya kufungua shule kama ilivyotajwa hapo juu.
   Mara mwanafunzi afikapo shuleni aripoti kwa **Mkuu wa Shule** kwa mapokezi na usajili. Mkuu wa shule atahakikisha kwamba mwanafunzi amekuja na stakabadhi iliyolipiwa kwenye benki ya **NMB A/c 30410008757** yenye jina la **Julius Kambarage Nyerere sekondari.**

**3. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**
**3.1 SARE YA SHULE**

**2. SARE ZA SHULE**

**a)** Sketi mbili(2) ndefu mpaka chini damu ya mzee za rinda box, mcholo wa sketi utaambanishwa , kitambaa kizito.(kama rangi na mshono wa sketi vitakuchanganya pia vinapatikana shuleni hivyo unaweza kuja siku ya kuripoti na ukashonewa huku)
**b) mashati mawili 2 meupe mikono mirefu**
**c)** Sweta mbili za kuvaa wakati wa baridi (zinapatinana hapa shuleni sh. **15000/=).**

**d) Viatu vya ngozi pea mbili visigino vifupi vya kamba**
**e)** Soksi nyeupe ndefu (stocking) pea mbili 2
**f)** Raba za michezo pea moja (1).
**g) Sketi ya blue fupimoja ya michezo na T-shirt ya blue ya michezo**
**h)** Track suti rangi ya blue pea moja zenye nembo ya shule (zinapatikana shulen Tsh.26,000)


**i)** T- shirt pea mbili rangi ya kijivu na nyeusi yenye nembo ya shule (zinapatikana shuleni tshirt moja tsh 15000/=

**j)** kwa waislamu shona kijuba cheupe utakachovalia kwenye sare ya shule. Na cheusi utakachovalia shamba dress

**k) Kwa wenye matatizo ya kiafya yaliyothibitishwa na daktari waje na jacket zito la rangi nyeusi kwa ajili ya kuvaa kipindi cha baridi kali.**

**l) Vazi la kulalia rangi nyeupe au blue.**

**m)** Shamba dress nzito isiyopitisha mwanga pea mbili rangi ya pinki mshono wa rinda box ndefu mpaka chini kitambaa kizito(gauni lakuvaa wakati kazi za usafi na nje ya masomo) yanapatikana shuleni Tsh.35,000/= mshono umeambatanishwa.



***ANGALIZO:Nguo zote za kiraia haziruhusiwi kabisa kuvaliwa shuleni, hivyo mwanafunzi aje na sare (uniform) za kutosha kwa matumizi yake ya kila siku awapo shuleni. Wakati wote mwanafunzi awapo shuleni,safarini, katika mazingira na wakati husika, mwanafunzi anatakiwa kuvaa sare ya shule tu.***

### 3.2 ADA NA MICHANGO YA SHULE

| AINA YA MALIPO | | MUHULA WA I | MUHULA WA II | JUMLA KWA MWAKA |
|---|---|---|---|---|
| **a) Ada** | | Tsh 35,000/= | Tsh 35,000/= | **Tsh 70,000/=** |
| **b) Michango Inayotakiwa Kulipwa na Kila Mzazi** | | | | |
| i | Ukarabati | Tsh 15,000/= | - | Tsh 15,000/= |
| ii | Kitambulisho na picha | Tsh 6,000/= | - | Tsh 6,000/= |
| iii | Taaluma | Tsh 20,000/= | - | Tsh 20,000/= |
| iv | Wapishi, Walinzi na Wafanyakazi wengine | Tsh 30,000/= | - | Tsh 30,000/= |
| v | Nembo (02) | Tsh 4000/= | - | Tsh 4000/= |
| vi | Huduma ya kwanza na Bima ya afya | Tsh 10,000/= | - | Tsh 10,000/= |
| vii | Tahadhari | Tsh 5000/= | - | Tsh 5000/= |
| viii | Joint exams (Mock) | - | Tsh 20,000/= | Tsh 20,000/= |
| ix | Umeme | Tsh 8,000/= | - | Tsh 8,000/= |
| **JUMLA** | | Tsh **133,000/=** | **Tsh 55,000/=** | Tsh **188,000/=** |

### 3.3 MAHITAJI MUHIMU AMBAYO MWANAFUNZI ANAPASWA KULETA SHULENI

i. Ream ya karatasi 2 double A-4(kwa mwaka)
ii. Jembe 1

iii. Fyekeo 1
iv. Reki 1
v. Soft broom 1 ,Hard broom1 na sikuiza 1
vi. Ndoo ya lita 20 (1) kwa matumizi ya shule tu.
vii. Dawa ya choo lita 5Pamoja na dawa ya Mbu (HIT) 750ML chupa mbili (02)
viii. File mbili la kutunzia kumbukumbu zake ofsini(Aina ya spring file plastic ). Na **ALBA (RADO)** la kutunzia nyaraka zake.
ix. Picha (Passport) nne za wazazi/walezi watakaoruhusiwa kumtembelea mwanafunzi shuleni.
x. Nakala ya cheti cha kuzaliwa
xi. Nakala ya matokeo (result slip)
xii. Bima ya afya kama anayo`

## 3.4 MAHITAJI AMBAYO MWANAFUNZI ANAPASWA KUWA NAYO KWA MATUMIZI YAKE BWENINI

**i.** Shuka mbili (02) moja ya rangi ya pink na nyingine bluu (light blue) aje nazo.
ii. Mto na foronya aje nao.
iii. Ndala/ kandambili aje nazo.
iv. Sanduku la bati kwa ajili ya kutunzia vifaa vyake ( ni lazima aje nalo toka nyumbani).
v. Chandarua aje nacho
vi. Taulo aje nayo.
vii. Ndoo ya kuchotea maji, beseni la kuogea na Dumu la lita 5 la kutunzia maji yake ya kunywa. (aje navyo).
viii. Fedha kidogo za matumizi yake muhimu ya kila siku (aje nayo)
ix. Toilet paper 10 kwa matumizi yake (aje nazo).
x. Sahani, bakuli, kijiko na kikombe cha nusu lita aje navyo.
xi. Aje na blanketi lake la kujifunika kwa sababu ya baridi (Mashuka ya kimasai, vikoi n.k hayataruhusiwa kabisa, na mwanafunzi akikutwa nayo atachukuliwa hatua za kinidhamu ikiwa ni pamoja na kuteketezwa mashuka hayo).
xii. Aje na godoro futi 3.
xiii. Cheti cha ugonjwa kama anacho.
xiv. Pedi pakt 6

xv. Vitabu vya masomo kwa Tahasusi husika(Combination). Mfano kwa shule hii ni **HGL**na **HGK**hivyo mwanafunzi anunue vitabu kulingana na tahasusi aliyo pangiwa.

## 3.5 VIFAA VYA KUTUMIA DARASANI (AJE NAVYO).

**i.** Kikokotozi (calculator) aje nacho ni lazima kitakaguliwa
ii. Mathematical set (aje nalo ni lazima litakaguliwa)
iii. Rula, kalamu na penseli.
iv. Madaftari makubwa (counter book) yasiyopungua kumi 10.
v. Kwa **HGL** waje na Dictionary (Oxford Advanced Learner’s Dictionary)
vi. **Pia unashauriwa kununua vitabu viwili kwenye Tahasusi unayosoma**; **mfano HGL-Englishna Geographyau History 1**.

## 4. SHERIA ZA SHULE

### 4.1 MAKOSA YAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE MARA MOJA

i. Wizi
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku **90** bila taarifa/utoro
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla.
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au na mtu yeyote Yule
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule
vii. Kufuga ndevu
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya
ix. Uvutaji sigara
x. Uasherati, mahusiano wa jinsia moja, kuoa au kuolewa
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba
xii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi
xiii. Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana
xiv. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule
xvi. Kudharau bendera ya taifa
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama vile kunywa sumu n.k
xviii. Uharibifu wa mali ya umma

### 4.2 MAMBO AMBAYO MWANAFUNZI HARUHUSIWI KUFANYA AWAPO SHULENI.

i. Kufuga kucha ndefu na nywele ndefu
ii. Kufuga ndevu
iii. Kuvaa mavazi yasiyo sare rasmi ya shule
iv. Kugombana/ ugomvi
v. Kuiga mitindo ya kihuni/isiyofaa
vi. Kuchubua ngozi ya mwili kwa kutumia madawa
vii. Kwenda nje ya shule bila kuvaa sare ya shule
viii. Kwenda nje ya shule bila ruhusa
ix. Kuvaa kofia, bangili, na mapambo mengine yasiyo sehemu ya sare ya shule.
x. Kuwa na simu, kamera na redio shuleni.
xi. Kutembelewa na wageni zaidi ya mara moja kwa mwezi.
xii. Kula chakulanjeyabwalo bila ruhusa.
xiii. Kukiuka ratiba au utaratibu wa shule.
xiv. Kupeleka wageni bwenini.
xv. Kwenda kwenye nyumba za walimu au wafanyakazi wengine bila ruhusa/sababu muhimu.

5. **VIAMBATANISHO NA FOMU MUHIMU**
   a) Fomu ya kiapo cha Mwanafunzi na kiapo cha Mzazi/Mlezi.
   b) Fomu ya historia ya mwanafunzi na maelezo binafsi kuhusu mwanafunzi.
   c) Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya Serikali.
   d) Nakala za **Result slip** na **cheti cha kuzaliwa**.

   ***N:B Fomu hizi baada ya kujazwa kikamilifu lazima zirejeshwe shuleni wakati mwanafunzi anaporipoti na zitakaguliwa.***

   ***MUHIMU:***
   i) Shule haipokei fedha taslimu. Malipo yote yalipwe benki na mwanafunzi aje na stakabadhi ya malipo ya benki **NMB A/c 304100027887** yenye jina la **Julius Kambarage Nyerere.**
   ii) Mzazi/Mlezi hakikisha kuwa mwanao anakuja na vitu anavyotakiwa kuwa navyo. Hatutampokea mwanafunzi yeyote ambaye hatakuja na vifaa vinavyotakiwa na kutokulipa michango kikamilifu kama inavyoonyesha katika "Joining instruction) (fomu ya kujiunga).
   iii) Simu za mkononi/ kiganjani, pasi na redio haziruhusiwi kabisa shuleni kwa mwanafunzi. Mwanafunzi asije navyo. Akija na simu na akakamatwa nayo, sheria itachukua mkondo wake ikiwemo kufukuzwa shule pamoja na kuteketezwa simu.
   iv) Mzazi /Mlezi kumbuka kwamba ili mwanafunzi aweze kufikia malengo yake ya kitaaluma, anapaswa pia awe anasoma vitabu. Shule haina vitabu vya kutosha vya A – Level. Hivyo basi unaagizwa kumnunulia mwanao vitabu vya masomo atakayosoma kulingana na silabasi ya sasa.
   v) Ndugu Mzazi/Mlezi, shule hii haitoi kabisa chakula tofauti na kile kinachotumiwa na wanafunzi wote, kwa mwanafunzi mmoja mmoja (special diet), vyakula vinavyotumika hapa ni ugali, wali, maharage pia nyama na mboga za majani kadri vitakavyopatikana kulingana na mazingira yenyewe.

6. Tafadhali soma kwa makini maelezo/ maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**……………………………**

**Melesian J.Gerald**

**MKUU WA SHULE**

*Kiambatanisho A*

## KIAPO CHA MWANAFUNZI.

Mimi (jina la mwanafunzi) ………………………………………………………… nakubali kwa dhati kabisa nafasi niliyopewa na Taifa kujiunga na shule hii. Naahidi kufuata sheria za shule na taratibu zote kama zilivyotolewa na zitakavyotolewa na uongozi wa shule.

Jina la mwanafunzi …………………………………………………………

Saini ………………………………………………….. Tarehe ……………………………….

## KIAPO CHA MZAZI/ MLEZI.

Mimi (Jina la mzazi/mlezi) ………………………………………………………. Ambaye ni Mzazi/Mleziwa (Jina la mwanafunzi) …………………………………………………….. nimeyasoma na nimekubaliana na masharti na sheriazaShuleyaSekondari Julius kambarage Nyerere ambakokijanawanguamechaguliwakujiunga. Naahidikwambanitamhimizamwanangukufuatasheria na taratibuzotezashule. Pia naahidikushirikiana na uongoziwashulekatikamalezi bora yamwananguilibaadaeawe raia bora na mwemawa Taifa letu.

Aidhanaahidikuwanitamlipia na kumpatiamwananguhudumamuhimuzashulekama vile; Ada na Michango; Sare zashule na michezo; Matibabu; Vifaavyakujifunziaikiwa ni pamoja na madaftari, kalamu, vitabu n.k

Jina la Mzazi/Mlezi …………………………………….;..….. Namba ya simu …………………

Mtaa (Kitongoji) ………………………………………………….. Kijiji …………………….

Anuani: S.L. P ……………………………………………. Wilaya …………………………….

SahihiyaMzazi/Mlezi ……………………………………… Tarehe …………………………..

*Kiambatanisho B*

**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA TAMISEMI**

**JULIUS KAMBARAGE NYERERE.**

**HISTORIA/TAARIFA YA MWANAFUNZI.**

1. Jina la kwanza ……………… Jina la kati …………………
   Jina la mwisho …………………
2. Jina la Mzazi/Mlezi ………………………………………………………
3. Kama ni Mlezi: uhusiano …………………………………………………………
4. Namba za simu za Mzazi/ Mlezi ………………………………………….
5. Anwani ya kudumu ya Mzazi/Mlezi ………………………………………..
6. Mahali mwanafunzi alipozaliwa: Kijiji cha ……………………………… Kata ya ……………………….
   Wilaya …………………….. Mkoa …………….
7. Dini ……………………………………… Dhehebu ……………………………..
8. Unaingia kidato cha ………………….. Tarehe/Mwaka ……………………
9. Kutoka shule ya Msingi/Sekondari ………………………………………….. Wilaya ……………………………………… Mkoa …………………………………
10. Kazi anayofanya Mzazi/Mlezi wako ni …………………………. Mahali ……………………………
11. Usafiri kutoka hapa shuleni hadi nyumbani kwenu ni: (Toa maelezo)
    - ………………………………………………………………………………
    - ………………………………………………………………………………
12. Ndugu wengine ambao wanaweza kupelekewa habari muhimu juu yako au masuala ya shuleni ni:-

| Jina la ndugu | Uhusiano | Namba za simu |
|---|---|---|
| i) | | |
| ii) | | |
| iii) | | |

13. Unalipiwa/utalipiwa karo na: Taja jina na anwani yake, au namba za simu ……………………………………………………………………………………………..
14. Taarifa za wazazi: A. Wapo ☐ B. Wamefariki ☐ (weka vema ( √ ) panapohusika)
15. Kabla hujaja hapa shuleni umepimwa na daktari? ndiyo/hapana. ni ugonjwa upi ni wakudumu kwako? ……………………………………….
16. Sifa maalumu kama unazo ……………………………………………………...

**17. Nakili kuwa maelezo niliyotoa hapo juu ni sahihi.**

**……………………………..** **…………………………….**

**Saini ya Mwanafunzi** **Saini ya Mzazi/Mlezi**

***Kiambatanisho C***

**MINISTRY OF EDUCATION, SCIENCE, TECHNOLOGY AND VOCATIONAL TRAINING**
**JULIUS KAMBARAGE NYERERE SECONDARY SCHOOL**

**MEDICAL EXAMINATION FORM.**

Full name ………………………………………………………………………………………

Age …………………….. Height (in cms) …………………… Weight (in kgs) ……………

1. Blood count ………………………………….. (Red and White) ………………………...
2. Stool Examination ……………………………………………………………………
3. Urine Analysis ………………………………………………………………………..
4. Syphilis and other V.D ……………………………………………………………….
5. T.B and Leprosy Test ………………………………………………………………...
6. Eye Test ………………………………………………………………………………
7. Ear Test ………………………………………………………………………………
8. Chest test ……………………………………………………………………………..
9. Abdominal Test ………………………………………………………………………
10. Blood Group (very crucial) …………………………………………………………..
11. Spleen ………………………………………………………………………………...
12. H.I.V Test, Positive ……………………. Negative ……………… (Tick where necessary)

    Additional information e.g Physical defects or impairments infection chronic or family Diseases (eg Sickle cell).

    ……………………………………………………………………………………………

    ……………………………………………………………………………………………

    …………………………………………………………

    I certify that the above student is fit/pursues Secondary Education

    Signature ………………………………

    Designation ……………………………

    Station …………………………………

    Date ……………………